



OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM



**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA**

Mkurugezi wa Jiji la Dar es Salaam anawatangazia Watanzania wote wenye sifa, nafasi za kazi za muda zifuatazo katika Halmashauri ya Jiji:-

**FUNDI SANIFU WA BAHARINI DARAJA LA II (NAFASI I) – TGS C**

**SIFA:**

1. Awe na Stashahada kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali

*Kazi za kufanya:*

- i. Kuisimamia uendeshaji wa injini za maboti
- ii. Kutunza injini za maboti
- iii. Kufundisha mafunzo katika fani ya ufundisanifu wa baharini kwa vitendo katika vyuo vya uvuvi
- iv. Kuchunguza, kutambua na kufanya marekebisho ya mitambo ya baharini.

**DEREVA MASHUA /KIVUKO DARAJA LA II-TGOS A – (NAFASI 1)**

- Awe na cheti cha Kidato cha IV
- Awe na Cheti cha Udereva kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali

*Kazi za kufanya:*

- a) Kufunga na kufungua kamba za Mashua/Kivuko
- b) Kuchunga usalama wa abiria na Magali yaliomo ndani ya Mashua/Kivuko
- c) Kupanga Abiria au Magari kwenye Mashua /Kivuko
- d) Kuendesha na Kuongoza Mashua/Kivuko
- e) Kutunza Daftari za safari ya Mashua/Kivuko
- f) Kuhakikisha kwamba Injini za Kivuko zipo katika hali nzuri ya kufanya kazi
- g) Kuangalia Mafuta na vyombo vingine vya kufanyia kazi



## **MASHARTI YA JUMLA:**

1. Awe na cheti cha uraia/namba ya NIDA.
2. Awe na cheti cha kuzaliwa.
3. Awe na umri kati ya miaka 18-45.
4. Awe amehitimu na kupata cheti cha elimu (**Results Slip**) hazitakubalika.
5. Watumishi waliopunguzwa kazi/kufukuzwa kazi/Kuachishwa kazi kwa sababu ya kughushi vyeti serikalini hawaruhusiwi kuomba.
6. Ajira ni ya mkataba wa mwaka mmoja, mkataba unaweza kurudiwa iwapo Mwajiri ataridhishwa na utendaji wa Mtumishi.

## **Barua zote ziambatane na nyaraka zifuatazo:**

Nakala za vyeti vya mwombaji vilivyothibitishwa ambayo ni:

- Cheti cha , kidato cha nne au zaidi
- Cheti cha Taaluma
- Cheti cha Kuzaliwa.
- Kitambulisho cha Taifa/kupigia kura
- Cheti cha daktari cha kuthibitisha afya
- Picha ndogo mbili (2) za rangi (colored Passport size) za hivi karibuni.
- Waombaji wenye sifa pungufu au za juu hawaruhusiwi kuomba kwani maombi yao hayatafanyiwa kazi.

Barua ambazo hazikuambatanishwa na nyaraka zilizotajwa hapo juu hazitashughulikiwa.

## **JINSI YA KUTUMA MAOMBI:**

Barua zote za maombi **ziandikwe kwa mkono** zikiwa na anwani kamili ya mwombaji pamoja na namba ya simu zikitaja nafasi unayoomba zitumwe kwa anuani ifuatayo:

## **MKURUGENZI WA JIJI**


**HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM**

**S.L.P. 20950**

**DAR ES SALAAM.**

Barua za maombi ziwasilishwe Ofisi ya masjala ya Mkurugenzi iliyopo Mtaa wa Mission karibu na jengo la Bandari.

Mwisho kupokea maombi ni tarehe 06/01/2023 Ijumaa saa 9.30 Mchana.



Eng. Amani I.B. Mafuru

**KAIMU MKURUGENZI WA JIJI LA DAR ES SALAAM**